



# WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI (RITA)



## TAARIFA KWA UMMA

### UTARATIBU WA KUHAKIKI VYETI VYA KUZALIWA NA VIFO KWA WAOMBAJI WA MIKOPO YA ELIMU YA JUU KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhadini (RITA) umeanza Uhakiki wa Vyeti vya Kuzaliwa na vyeti vya vifo (ikiwa muombaji amepoteza mzazi mmoja au wote) vya waombaji wanaotarajiwa kuomba mikopo ya masomo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka 2019/2020. **Maombi yote yatafanyika kwa njia ya mtandao pekee.**

Waombaji wanaohakiki wanatakiwa kufuata maelezo yafuatayo:

- 1- Kila muombaji aingie katika mtandao kwa anuani: <http://uhakiki.rita.go.tz/uhakiki> ili kujisajili na kupata akaunti maalumu ambayo atatumia kutuma nakala ya cheti kinachohakikiwa, namba ya uthibitisho wa malipo/ risiti (*ambayo atatumia kwa ujumbe wa simu malipo yanapokamilika*) na kupokea nakala ya cheti kilichohakikiwa.
- 2- Ada ya uhakiki kwa kila cheti ni TShs. 3,000/= (elfu tatu) ambayo italipwa kwa njia mojawapo kati ya zifuatazo:
  - » Kupitia Benki au Mawakala wa Benki ya NMB au CRDB kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo (*control number*) **991380913455**.
  - » Kulipia kwa njia ya Simu ya Mkononi kama ifuatavyo:
    - Fungua menu ya M Pesa; Tigo Pesa; Airtel Money; T Pesa (TTCL Pesa) au Halopesa
    - Chagua "Lipa Bill" kulingana na mtandao unaotumia
    - Chagua "Malipo ya Serikali"
    - Ingiza "Control Number" ambayo ni **991380913455**
    - Ingiza kiasi unacholipia (**TShs. 3,000/= tu**)
    - Ingiza namba yako ya siri
    - Thibitisha malipo

Malipo yatakuwa yamekamilika baada ya muombaji kupokea risiti kwa njia ya ujumbe wa simu kutoka namba **GePg** kupitia namba aliyotumia kufanya malipo au namba aliyoulizwa na mhudumu wa benki/wakala.

#### MUHIMU:

- » Kila muombaji afungue akaunti binafsi ya uhakiki na atunze nywila (password) ya akaunti yake.
- » Tuma kivuli cha cheti kinachosomeka vizuri na hakikisha namba ya ingizo (entry number) inasomeka vizuri.
- » Utapokea ujumbe wa kukiri kupokea nyaraka zako kwa maombi yaliyotumwa kikamilifu.
- » Majibu ya uhakiki yatatumwa katika akaunti uliyofungua.
- » Waombaji waliohakikiwa mwaka jana na vyeti vyao kuthibitishwa ni halali hawatakiwi kurudia uhakiki

**Kwa maswali na maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia:**  
**Simu:** 0800117482 (*bila malipo*) / **Barua pepe:** [Info@rita.go.tz](mailto:Info@rita.go.tz)  
[www.rita.go.tz](http://www.rita.go.tz) | [www.facebook.com/ritatanzania](https://www.facebook.com/ritatanzania)

**Imetolewa na: Kitengo cha Masoko na Mawasiliano - RITA**